

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Kingóla,
S.L.P 845,
67109 MOROGORO
Mob: 0738150143
Simu: 023-2614302
Nukushi: 023-2614478
Simu ya Bure: 113 au *113#
Barua pepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MOROGORO Septemba 17, 2020

TAKUKURU YAREJESHA MATOFALI KWA WANAKIJJI.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro imeendelea kupigania haki za wanyonge kwa kufanikiwa kurejesha matofali zaidi ya **Elfu Kumi na Mbili na Mia Nne (12,400)** kwa wanakijiji wa Pulambili katika Kata ya Kidugalo Mkoani Morogoro.

Urejeshwaji huo unafuatia malalamiko yaliyowasilishwa TAKUKURU mnamo mwezi Julai, 2020 ambapo ilidaiwa kuwa fedha za wanakijiji wa Pulambili zilizokusanywa kutokana na mauzo ya viwanja vya kijiji kisha kukabidhiwa kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Pulambili zimefanyiwa ubadhirifu.

Uchunguzi wa taarifa hiyo ulianza mara moja ambapo ilibaini kuwa; Mnamo mwaka 2019 wanakijiji wa Pulambili walikubaliana kutenga eneo lililokuwa linamilikiwa na Serikali ya kijiji hicho kwa ajili ya upimaji wa viwanja vya makazi na biashara ili viuzwe. Lengo la uuzwaji wa viwanja hivyo lilikusudiwa kuwa ni kukusanya fedha kwa ajili ya maendeleo ya kijiji hususani ujenzi wa shule ya msingi Pulambili kwa kuzingatia kuwa Kijiji hicho hakina shule.

Ilibainika kuwa iliridhiwa kuwa viwanja hivyo viuzwe kwa Shilingi **Elfu Hamsini (50,000/=)** ambapo kati ya fedha hizo Shilingi **Elfu Thelathini na Tano (35,000/=)** ni gharama za ununuzi wa viwanja na Shilingi **Elfu Kumi na Tano (15,000/=)** ni gharama ya upimaji.

Zoezi zima la uuzaji wa viwanja hivyo liliratibiwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha **Pulambili Bw. Juasin Charles Furahisha** kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Kitongoji cha **Pulambili "A"** aitwaye **Ally Mrisho Mgya** maarufu kama **PesaMaua**.

Ilibainika pia kuwa katika utekelezaji wa zoezi hilo viwanja 53 vilipimwa na kuuzwa kwa wanakijiji mbalimbali na fedha kiasi cha Shilingi **Milioni Moja Mia Nane na Hamsini na Tano Elfu (1,855,000)** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi **Laki Sita na Kumi na Tano Elfu (615,000/=)** pekee ndizo zilizowasilishwa katika ofisi ya kijiji cha Pulambili.

TAKUKURU ilibaini kuwa kiasi cha shilingi **Milioni Moja Mia Mbili na Arobaini Elfu (1,240,000/=)** taarifa zake hazikuwasilishwa katika ofisi ya kijiji.

Aliyekuwa na dhamana ya kupokea fedha hizo ni Mwenyekiti wa kijiji. Kukosekana kwa fedha hizo ni Dhahiri kuwa mwenye dhamana alivunja uaminifu na kufanya maumizi binafsi kinyume na matarajio ya lengo zuri la wananchi waliokusudia kuisaidia Serikali yao kujileta maendeleo yao.

Kwa kuwa lengo lilikuwa ni kupata matofali kwa ajili ya ujenzi wa shule na ili kuhakikisha kuwa jasho la wananchi wanyonge linalindwa na kuleta manufaa kwao, TAKUKURU mkoa wa Morogoro, ilimwamuru mwenyekiti huyo afyatue matofali yenye thamani ya fedha alizozifanyia ubadhirifu ili lengo la kujenga ya shule ya msingi lifikiwe na azma ya watoto wanyonge wa wananchi wanyonge waliojitolea kwa hali na mali liweze kutimia

Hivyo, leo tutakabidhi jumla ya **matofali 12,400** ambayo yamefyatuliwa na Mwenyekiti **Bw. Juasin Charles Furahisha** ili yatumike kama sehemu ya ujenzi wa shule ya msingi iliyokusudiwa na wananchi.

Ni Imani ya TAKUKURU mkoa wa Morogoro kuwa urejeshwaji wa tofali hizo utawatia nguvu na ari kubwa wananchi wa Kijiji cha Pulambili kuwahikisha kuwa wanakamilisha ujenzi wa boma la shule hiyo haraka. TAKUKURU mkoa wa Morogoro inawahakikishia wananchi wa Kijiji cha Pulambili kuwa watasimamia kila senti itakayochangwa na wananchi kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa shule inatumika ipasavyo.

TAKUKURU mkoa wa Morogoro haitasita kuchukua hatua kwa mtu yeyote atakayejihusisha na ubadhirifu wa mali za umma husuani fedha zinazochangwa na wananchi wanyonge kwa lengo la kujiletea maendeleo, hivyo rai inatolewa kwa viongozi waliopewa dhamana kuhakikisha wanasimamia michango ya wapenda maendeleo kwa uaminifu na uadilifu.

Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza.

Imetolewa na:

Janeth Machulya

Mkuu wa TAKUKURU (M),

Morogoro.
